ISO 9001:2015 Certified

# The Regulator

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Linatolewa bure

ISSN: 0856 - 8030 | TOLEO NAMBA 1/2025 | JANUARI - MACHI 2025




# Tathmini mpya maudhui ya ndani Utangazaji

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Taasisi yenye viwango vya ISO 9001: 2015

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni taasisi iliyoasisiwa kwa mujibu wa sheria kusimamia sekta ya mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Tanzania.

## DIRA

Jamii iliyowezeshwa na huduma za mawasiliano.

## DHIMA

Kusimamia huduma za mawasiliano kwa ustawi wa jamii ya Tanzania.

## WAJIBU

Wajibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni kusimamia sekta ya mawasiliano na kielektroni na posta kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania Namba 12 ya mwaka 2003.

## TUNU KUU

1. **Weledi:** Tunatekeleza majukumu yetu kwa kutoa huduma bora tukizingatia maadili na heshima kwa wateja wetu;

2. **Utendaji wa pamoja:** Tunaamini katika utendaji kazi wa pamoja ili kutatua matatizo na kutambua kwamba mawasiliano imara ni muhimu katika kujenga mazingira ya ushirikiano;

3. **Ubunifu:** Tunazingatia ubunifu katika kushughulikia masuala ya kiudhibiti sanjari na mabadiliko ya teknolojia duniani;

4. **Uwajibikaji:** Tunawajibika kikamilifu na kuchukua dhamana tunapotoa huduma;

5. **Uadilifu:** Tunatekeleza kazi zetu kwa kuzingatia maadili, uthabiti na uaminifu wa hali ya juu.

## Anwani za TCRA

**Makao Makuu**
Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, 14414 Dar es Salaam S.L.P 474
Simu: 0800008272 / +255 22 2199760 - 9 / +255 22 2412011 - 2 / +255 784558270 - 1
Baruapepe:barua@tcra.go.tz

### Ofisi za Zanzibar na Kanda

**Ofisi ya Zanzibar**
19 Mtaa wa Mbuyukisutu, Chukwani,
71194 Mjini Magharibi. S.L.P 3284, Zanzibar
Simu: 0800008272 / +255 24 2235062
Baruapepe:zanzibar@tcra.go.tz

**Kanda ya Ziwa**
Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya 4,
Upande B, 13 Barabara ya Jomo Kenyatta
33194 Mwanza. S.L.P 3108
Simu: 0800008272 / +255 28 2505082
Baruapepe: mwanza@tcra.go.tz

**Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 5, 7 Barabara ya Karume, 53194 Mbeya. S.L.P 1375
Simu: 0800008272 / +255 25 2505016
Baruapepe: mbeya@tcra.go.tz

**Kanda ya Mashariki**
147 Barabara ya Kajenge, 14194 Dar es Salaam
S.L.P 33613. Simu: 0800008272 / +255 22 2775110 / +255 22 2775114. Baruapepe: easternzone@tcra.go.tz

**Kanda ya Kaskazini**
Jengo la PAPU, Ghorofa ya 12, 280 Barabara ya Moshi - Arusha. 23194 Arusha. S.L.P 15675
Simu: 0800008272 / +255 27 2611430
Baruapepe: arusha@tcra.go.tz

**Kanda ya Kati**
Jengo la PSSSF, Ghorofa ya 4, 2 Mtaa wa LAPF,
41194 Dodoma. S.L.P 2229,
Simu: 0800008272 / +255 26 2321731
Baruapepe: dodoma@tcra.go.tz

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 1/2025. JANUARI - MACHI, 2025

The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyoanzisha TCRA inaipa Mamlaka wajibu katika majukumu yafuatayo:

1. Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda maslahi ya watumiaji;
3. Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi;
4. Kukuza upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu;
5. Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:
   (i) Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;
   (ii) Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na
   (iii) Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## MKAKATI WA TCRA 2021/22-2025/26 NA MALENGO YA KIMKAKATI

Mamlaka imeandaa malengo mbalimbali ili kufikia maono yake katika kukabiliana na mambo muhimu kama yalivyobainishwa katika uchambuzi wa hali halisi ya kisekta. Malengo hayo ni:-

1. Kukuza miundombinu na huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta yenye usalama, ufanisi na imara;
2. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta zenye ubora na unafuu;
3. Kuimarisha ubunifu wa huduma zinazodhibitiwa, uandaaji wa maudhui ya ndani na ujanibishaji;
4. Kuimarisha ufanisi wa huduma zinazodhibitiwa na kuwalinda wadau; na
5. Kuimarisha uwezo wa taasisi.

## MATOKEO YA MKAKATI

1. Kupatikana kwa huduma za mawasiliano za uhakika na salama;
2. Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu;
3. Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
4. Kukua kwa ufanisi wa sekta ya mawasiliano na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo, kanuni ndogo na viwango kwa wadau wa sekta ya mawasiliano; na
5. Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.

## SERA YA UBORA

Kutokana na nguvu za kisheria za kusimamia sekta za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta Tanzania, TCRA imejizatiti kuweka mazingira mazuri kwa wenye leseni kwa kutoa rasilimali, kudumisha na kuendelea kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Ubora ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na nafuu kwa watumiaji ili kukidhi matakwa ya Sheria na ya kiudhibiti.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz;
dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania

# Yaliyomo

04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



11 Tanzania yajiandaa kuelekea utangazaji wa redio kidijitali



Matukio

05 Tathmini mpya maudhui ya ndani



Makala kuu

15 Mwelekeo ukuaji sekta kupita malengo ya Serikali




Ripoti

10 Mikakati TCRA kuendeleza maudhui ya ndani



Utangazaji

19 Takwimu sekta ya Mawasiliano



BARUA YA MHARIRI

# Maudhui ya ndani muhimu kwa ustawi wa Watanzania

Usimamizi wa huduma za maudhui ni mojawapo ya majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Mpango mkakati wa TCRA unaoendelezwa kila wakati, unataja hatua za kuwezesha kuwepo huduma za utangazaji zilizo imara na thabiti Tanzania.

Mpango huo pia una lengo la kujenga jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani. Aidha, masuala muhimu kwenye Mkakati huo ni pamoja na kuchangia kujenga jamii inayowezeshwa na huduma za mawasiliano.

Haya yanayotokana na dhima ya TCRA, ambayo ni kusimamia huduma za mawasiliano kwa ustawi wa jamii ya Kitanzania. Maudhui bora ya utangazaji yanachangia ustawi wa Watanzania kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Taarifa sahihi na maudhui yanayohusu shughuli za uchumi kunawezesha wawekezaji wa ngazi mbalimbali kufuatilia fursa na hivyo kuchangia kwenye kujenga uchumi.

Utoaji wa maudhui, kama ilivyo kwa huduma za mawasiliano ya simu pia hutoa fursa za ajira na ujasiriamali kwenye mfumo wote wa utoaji huduma.

TCRA inasimamia maudhui kwa kutoa leseni za huduma za utangazaji, kuweka viwango vya utoaji huduma na miongozo mbalimbali. Vilevile inafuatilia uzingatiaji wa masharti ya leseni na kanuni za huduma zinazotolewa. Shughuli zote hizi zimetungiwa kanuni.

Toleo hili linazungumzia kwa kina shughuli hizi kwa kuzingatia kanuni zilizotungwa mahsusi kwa ajili yake. Mojawapo ni kanuni kuhusu maudhui ya ndani yanayotolewa na redio na televisheni.

Pamoja na kutathmini upya masuala ya maudhui ya ndani, toleo hili lina ripoti ya ukaguzi wa ubora wa huduma za utangazaji ambayo inaonesha mwelekeo mzuri kwenye uzingatiaji wa masharti ya kanuni za leseni, na za utangazaji wa redio na televisheni.

Taarifa ya robo mwaka Januari hadi Machi mwaka huu inang'ara. Mwaka huu ni wa mwisho wa utekelezaji wa ahadi za Serikali ndani ya miaka mitano kuanzia 2020 unaonesha ukuaji wa kasi wa sekta na kwenye maeneo mengi ya huduma.

Tunayo makala kuhusu matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwenye kutoa huduma kwa umma. Tunachambua namna teknolojia mpya zinavyoweza kutatua changamoto kwenye sekta, ikiwemo ya ulaghai mitandaoni.

Mojawapo ya malengo ya Mpango wa Tanzania ya Kidijitali ni kuwezesha matumizi ya teknolojia zinazojitokeza kuongeza ufanisi wa uendeshaji na utawala. Tunayo ripoti ya wataalamu inayopendekeza kwa serikali hatua mbalimbali za kisera na kiusimamizi zitakazowezesha kufikia lengo hili.

Mapendekezo yao yamesisitiza kuwa matumizi ya teknolojia yatawezesha serikali kufikia malengo yake ya kimkakati kwenye sekta mbalimbali.




Jarida hili linakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya na pia kupanua mtandao wako wa watu wenye weledi kama wewe. Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tuma barua pepe kwa

regulator.magazine@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz

Soma kujisajili

Tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu. Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni **0800008272.**

UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

# TEHAMA inavyowajenga wanafunzi wasichana



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

***Ujumbe huu umeandaliwa kwa ajili ya maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA mwaka huu.***

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaamini kuwa msingi wa maendeleo katika jambo lolote ni kupata mafunzo sahihi na kutumia taaluma wezeshi kwa manufaa binafsi na jamii kwa ujumla.

TCRA imeratibu mafunzo ya muda mfupi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa wanafunzi wa kike wa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu. Mafunzo haya yametolewa kwa nyakati tofauti kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za elimu.

Vilevile tumeendesha mafunzo kwa wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalum ngazi ya elimu ya sekondari. Lengo ni kupunguza tofauti iliyopo katika uwezeshwaji wa masomo ya Sayansi na TEHAMA.

Wanafunzi waliopatiwa mafunzo ya teknolojia za maroboti wameonekana kuwa na chachu ya kuendelea kujifunza masomo ya TEHAMA na kuendeleza bunifu zao za kiteknolojia ili kutatua changamoto katika jamii inayowazunguka.

Wanufaika wengine wa mafunzo hayo ni wanafunzi wa shule za awali mkoa wa Dar es Salaam. Hawa walipata mafunzo kwa vitendo kuhusu nadharia za sayansi, ikiwemo mzunguko wa umeme kupitia vitu ambavyo wanafanya na kutumia kila siku, kama vile matunda na michezo ya watoto.

Mafunzo hayo yalitangulia maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA tarehe 24 Aprili mwaka huu. Siku hii inalenga kuhimiza wanafunzi wasichana kupenda masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STUH – au STEM, kwa kifupisho kwa Kiingereza).

Mafunzo yanakusudia kuhamasisha wanafunzi wasichana kuanzia shule za awali hadi vyuo vikuu kupenda masomo hayo. Aidha yanalenga kuwajengea kujiamini na kuthubutu kuzichangamkia fursa zilizopo kwenye shughuli zinazohitaji umahiri kwenye masomo hayo.

Mafunzo kwa wasichana shule za msingi yalifanyika Mtwara, na yalihusu teknolojia za maroboti na namna zinavyoweza kutumika kutatua changamoto za kijamii. Wanafunzi wa shule za sekondari Unguja na Pemba walifundishwa teknolojia ya ndege nyuki ('droni').

Kwa vyuo vikuu, mafunzo yalishirikisha wanafunzi wa kike kutoka vyuo mbalimbali ambao walipata ujuzi wa teknolojia za data zinazoonesha sehemu na maeneo, yaani geospatial. Mafunzo yalifanyika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kwa kutambua umuhimu wa kuwajengea vijana uwezo na ujuzi wa kidijiti, hasa katika zama za uchumi wa kidijiti, TCRA inaendeleza jitihada za kuhamasisha uanzishwaji wa vilabu vya kidijiti kwenye shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu. Madhumuni ni kuwapa wanafunzi wa jinsia zote hamasa kuongeza ufahamu wa masuala ya teknolojia za kidijiti na kubuni miradi inayohusisha TEHAMA ili kutatua changamoto za jamii zinazowazunguka ikiwemo kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kijiditi.

Desemba 2024, TCRA ilifikisha ajenda ya vilabu vya kidijiti kwa umoja wa Wakuu wa shule wapatao 300 Zanzibar, na walimu wakuu 5,000 Tanzania Bara.

MAKALA KUU

# Tathmini mpya maudhui ya ndani

Na Mwandishi wetu

Matakwa ya kikanuni kuhusu kiasi cha ukomo wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya redio na televisheni yanahusishwa kimsingi moja kwa moja na sababu za kudhibiti maudhui ya utangazaji. Vipindi vyote vya redio na televisheni vimekusudiwa kukuza tamaduni na misingi ya taifa husika.

Utangazaji kwa ujumla pamoja na maudhui ya ndani unachangia hasa katika kukuza uchumi, kuhifadhi utamaduni, na kuimarisha utambulisho na malengo ya kitaifa.

Mifumo ya kisheria/ kikanuni ya udhibiti wa sekta ya utangazaji pamoja na ufafanuzi au tafsiri za maudhui ya ndani hutofautiana kati ya nchi na nchi.

Bila kujali namna ya kusimamia maudhui yanavyotolewa, usimamizi wa utangazaji unazingatia na kulenga teknolojia, ikiwa ni pamoja na masafa, miundombinu, vyombo vya kusambaza maudhui na maudhui yenyewe.

Masafa ya utangazaji ni raslimali adimu na yana ukomo. Maudhui yana athari kubwa kwenye maisha ya watu.

Mamlaka za usimamizi huzingatia na husimamia utekelezaji wa viwango, kanuni, sheria na miongozo inayohusu masafa ya redio, teknolojia na maudhui.

Vikiwa vyombo vya mawasiliano ya umma, redio na televisheni vina jukumu la kuelimisha, kuburudisha na kuhabarisha jamii. Kanuni zinabainisha na kueleza jinsi watoa huduma wanavyopaswa kutimiza lengo hili.

Utangazaji ni uundaji na usambazaji wa maudhui kwa hadhira kubwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, vyombo hivyo ni pamoja na redio, televisheni na Intaneti.

Utangazaji huwafikia watu wengi zaidi kwa wakati mmoja kuliko aina nyingine ya kutoa habari kwa umma.




*Mtangazaji wa redio TBC Taifa iliyopo Barabara ya Nyerere jijini Dar es Salaam, Salome Baptister akiwa katika studio za kisasa. Uwekezaji katika teknolojia za kidijiti unaongeza ubora wa matangazo na maudhui.*

Wanaojiunga na wasiojiunga na huduma hio pia wanaweza kufikiwa kwa urahisi. Hapa Tanzania, maudhui ya utangazaji hutolewa au hufikishwa kwa walengwa kupitia redio, televisheni kidijitali mfumo wa ardhini, televisheni za mfumo wa setilaiti, televisheni ya nyaya, na vyombo vya habari vya mtandaoni.

Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya Tanzania (EPOCA) inaeleza maudhui ya utangazaji kuwa ni taarifa kupitia mazungumzo au sauti nyingine, data, maandishi au picha, iwe za kawaida au jongefu, isipokuwa tu pale yanapopitishwa katika mawasiliano ya binafsi.

Huduma za utangazaji zinaenea maeneo mengi na zinafikia hadhira pana na watu wengi, bila kujali viwango vyao vya kusoma na kuandika. Benki ya Dunia inakadiria kuwa angalau asilimia 77 ya watu duniani wanapata teknolojia ya utangazaji kwa urahisi. [3]

Redio za Tanzania zinatangaza kwa kutumia masafa ya FM. Haya hutoa/huwasilisha urudufishaji sahihi zaidi wa sauti halisi za vipindi kuliko aina nyingine za utangazaji.

Kufikia Machi 20125 matangazo ya redio kwa FM yalikuwa yamefikia asilimia 81.5 ya watu nchini, huku yakienea kijiografia kwa asilimia 57.

Televisheni za kidijitali kwa mifumo ya ardhini zilifikia asilimia 58 ya watu na asilimia 33 ya maeneo ya nchi. Mawimbi ya utangazaji ya setilaiti hufunika nchi nzima.

## Usimamizi wa utangazaji

Utangazaji unasimamiwa kutokana na upekee wake. Wadhibiti au wasimamizi wa maudhui huweka wajibu/masharti kwa watoa huduma wa maudhui ya redio na televisheni kwa sababu wanatumia rasilimali adimu za taifa, kama vile masafa ya redio.

Maudhui yanayotangazwa/kuoneshwa kupitia redio na televisheni huathiri hadhira kwa njia mbalimbali. Yanaweza kuwaridhisha watazamaji/wasikilizaji au kuwaletea madhara binafsi. Vilevile, maudhui hayo yanaweza kuwa na athari kwa mshikamano wa kitaifa na maadili ya jamii.

Sheria ya EPOCA ina sehemu inayobainisha wajibu wa watoa huduma za maudhui waliopewa leseni kuhakikisha kuwa wanazingatia masharti haya.

**Mchoro 1. Rejea: Kifungu cha 104 cha EPOCA: Kanuni za maadili mema kwa watoa huduma za maudhui ya utangazaji**

| **104.-(1) Maadili mema yanayozungumziwa kwenye kifungu hiki:** |
|---|
| **a.** Yatahusu na kuwabana watoa huduma wote waliopata leseni ya kutoa maudhui; |
| **b.** Yatakataza utoaji wa maudhui yasiyofaa kama vile, matusi, ya uongo, ya kutisha, au maudhui mengine yanayokera kwa namna yoyote ile. |
| **(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1)(b), kanuni hizo za maadili mema zitalenga kufanikisha malengo yafuatayo-** |
| **a.** Kulinda watoto dhidi ya maudhui yasiyofaa; |
| **b.** Kuzuia maudhui yanayoweza kuhamasisha au kuchochea uhalifu yasitolewe na watoa huduma wa maudhui. |
| **c.** Uwasilishaji wa taarifa za habari kwa kina, usahihi, na bila kuegemea upande wowote; |
| **d.** Uwasilishaji wa maudhui ya kidini kwa njia yenye usawa na uwajibikaji; |
| **e.** Kulinda umma dhidi ya maudhui ya kuudhi au hatarishi; |
| **f.** Udhibiti unaofaa wa matangazo na udhamini; na |
| **g.** Kuzuia matumizi ya mbinu au njia za mawasiliano zinazowasilisha ujumbe kwa watazamaji au wasikilizaji, au kwa namna yoyote kuwashawishi kiakili, bila wao kujua au kuelewa kikamilifu kilichotokea, au zenye uwezo wa kufanya hivyo. |

Wasimamizi wanafuatilia uzingatiaji wa kanuni, maelekezo na miongozo ili kuhakikisha kwamba majukumu matatu ya utangazaji ambayo ni kutoa elimu, burudani, na taarifa yanatekelezwa kwa usahihi na bila upendeleo.

Usimamizi huo unalenga kuzuia utangazaji wa maudhui yanayoweza kuwadhuru watoto kihisia au kisaikolojia, na watu wazima dhidi ya maudhui yenye madhara au ya kuudhi na kukera. Kanuni pia zinalenga kuhakikisha kuwa faragha za watu zinaheshimiwa.

Watoa huduma za utangazaji, kama ilivyo kwa waendeshaji wa vyombo vyote vya habari, wana jukumu muhimu katika mchakato wa kidemokrasia wa nchi.

Wasimamizi wa vyombo vya habari husimamia uzingatiaji wa kanuni maalum zenye masharti na miongozo mbalimbali wakati wa uchaguzi. Tanzania hupitia upya uripoti wa uchaguzi wa kisiasa vipingi vya Uchaguzi Mkuu na wa Rais. [5]

Utangazaji pia huchangia kuendeleza na kukuza biashara kupitia matangazo ya kibiashara na vipindi maalum kama vile makala za kihabari, matangazo ya moja kwa moja na shughuli za uhamasishaji. Kanuni za utangazaji hulinda umma dhidi ya matangazo yasiyofaa na yasiyo na maadili.

Aidha huduma za utangazaji huleta manufaa katika mnyororo mzima wa uzalishaji na utoaji wa maudhui. Mfano ni ajira zinazozalishwa katika hatua za uandaaji, uchakataji, uratibu na usambazaji wa maudhui.

Kazi hizi zote zinasimamiwa ili kuhakikisha kuwa hadhira inapokea maudhui sahihi na yenye ubora unaotakiwa. [6]

Kanuni za maudhui pia zinalenga huhakikisha utangazaji hautumiki kuchochea uhalifu, vurugu au uvunjifu wa amani. Baadhi ya kanuni hizi huainisha aina ya maudhui yaliyokatazwa.(7)




Azma na juhudi za kuhifadhi tamaduni za kitaifa, kuimarisha na kukuza utambulisho wa taifa zimeongeza msukumo wa uhitaji wa maudhui ya ndani katika redio na televisheni.

**Maudhui ya ndani** ni vipindi vinavyoanzishwa na kuanzia ndani ya nchi husika, ambavyo vinaaksi tamaduni, simulizi na mitazamo ya wananchi wake.

Ingawa tafsiri ya maudhui hutofautiana kati ya mamlaka mbalimbali za udhibiti lakini kiini chake ni kuendeleza maadili ya kitaifa.

Tanzania inafafanua maudhui ya ndani kuwa ni vipindi vya redio na televisheni vinavyokidhi vipengele vinne: Kwanza ni lugha inayotumika, (maudhui yanapaswa kuwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza). Vilevile masuala yanayozungumziwa yawe ni yale yanayowahusu au kuwagusa Watanzania moja kwa moja.

Kipengele kingine ni umiliki wa mchakato wa uzalishaji. Watanzania wanatakiwa kumiliki angalau asilimia 40 ya hisa katika taasisi za uzalishaji. Aidha kuna ushiriki. Maudhui ya burudani yanachukuliwa kuwa ya ndani ikiwa wengi wa wahusika, wakiwemo wasanii, kwa maudhui ya burudani, ni Watanzania. Mahali kurekodipia pawe ndani ya Tanzania.

Zaidi ya hayo, mwandishi wa kipindi kinachotangazwa anatakiwa kuwa ni Mtanzania. Iwapo kipindi kimezalishwa kwa ushirikiano na nchi nyingine, asilimia 50 au zaidi ya wandishi wake lazima wawe Watanzania. Hata hivyo, maudhui ya ndani hayajumuishi habari za kila siku wala maoni ya kisiasa au kijamii. [8]

Kanuni za maudhui ya utangazaji wa redio na televisheni zinazitaka televisheni na chaneli zinazopatikana bure kurusha angalau asilimia 60 ya maudhui ya ndani. Asilimia 80 ya muziki unaorushwa unapaswa kuwa wa ndani.

Watoa huduma za utangazaji kundi redio na televisheni za jamii wanatakiwa kuhakikisha kwamba angalau asilimia 80 ya maudhui yao yawe ni ya ndani.

### Mchoro 2. Nchi nyingine za Afrika zinavyofafanua maudhui ya ndani

| | |
|---|---|
| **Kenya**  | Taarifa yoyote ya ndani (ujumbe mfupi, maudhui ya picha na maandishi na yanayofanana nayo) ambayo yamebuniwa au kutengenezwa na mtoa huduma na ambayo yanatumwa kwa watumiaji bure au kwa malipo. |
| | *Chanzo: Tovuti ya Mamlaka ya Mawasiliano Kenya (CA) –* *www.ca.go.ke* |
| **Afrika Kusini**  | Vipindi vinavyozalishwa chini ya usimamizi wa wabunifu ambao ni raia wa Afrika Kusini. Maudhui ya utangazaji (ya sauti au picha) ambayo yamezalishwa ndani ya tamaduni za Afrika Kusini au yana uhusiano wa moja kwa moja na nchi hiyo. Maudhui haya yanaaksi maisha ya umma katika vipengele vyote vya jamii husika. |
| | Ufafanuzi wa "Uzalishaji" unajumuisha matumizi ya rasilimali watu wa ndani kama vile waongozaji, waandishi, waigizaji na wahusika wa kusaidia. |
| | Pia hujumuisha uzalishaji na uchakataji wa vipindi kama vile uhariri wa mtandaoni, uboreshaji wa picha na sauti, utayarishaji wa mwisho |
| | *Chanzo: Tovuti ya Mamlaka ya Mawasiliano Afrika Kusini (ICASA) –* *https://www.icasa.org.za* |
| **Ghana**  | Vipindi vinavyozalishwa ndani ya Ghana kwa kutumia vipaji vya Waghana na rasilimali zao. |
| | Matumizi ya lugha zinazotumika ndani ya nchi hii katika utangazaji. |
| | Aidha, maudhui yanayokuza bidhaa na huduma za ndani, |
| | Pamoja na vipindi vinavyoakisi utamaduni, historia na maadili ya Waghana *Chanzo: Tovuti ya Mamlaka ya Mawasiliano Ghana (NCA) –* *https://nca.org.gh/* |
| **Nigeria**  | Kipindi chochote kinachozalishwa ndani ya Nigeria, kwa sehemu au kwa ujumla, kikitumia lugha za nchi hiyo. Wahusika na timu ya uzalishaji iwe ya watu wa Nigeria. Vilevile kipindi kiakisi utamaduni wa Nigeria. |
| | *Chanzo: Tovuti ya Tume ya Mawasiliano ya Nigeria (NCC) –* *https://www.ncc.gov.ng/* |

Nixon Kariith, akiandika katika chapisho la "Sera na Utaratibu wa Kutangaza Afrika: Masuala yaMaudhui ya Ndani ya Vyombo vya Habari vya Utangazaji," anasema kuwa viwango vya maudhui ya ndani ni mbinu muhimu ya kukuza utofauti katika vipindi vya utangazaji. [10]

Kwa mujibu wa Nicholas Omuon, maudhui ya ndani huimarisha tamaduni za kitaifa kwa kuwa yanawakumbusha wanajamii kila mara kuhusu urithi wao wa kitamaduni. (11)

Uzalishaji wa maudhui ya ndani huchangia kuunda ajira katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji. Sekta ya vyombo vya habari na burudani huuchochea uchumi kwa kukuza vipaji vya ndani. [12]

Aidha, maudhui haya hukuza na kuhifadhi lugha za asili za maeneo husika, mila, na urithi wa kitamaduni na kuwapa hadhira maudhui yanayohusiana na muktadha na maslahi yao binafsi.

Maudhui ya ndani huchangia kuongeza utofauti wa vipindi na maudhui ya vyombo vya habari. Kanuni za maudhui zinazunngumzia masuala ya hadhira na vigezo vya kitamaduni, kijamii na kiuchumi.

Dkt. Elisha Magolanga wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anasema kuwa licha ya kuibuka kwa vipaji vya uundaji wa maudhui na kuongezeka kwa mahitaji ya filamu, uzalishaji wa maudhui ya ndani yenye ubora Tanzania unakabiliwa na changamoto nyingi.

Miongoni mwa changamoto hizo ni ukosefu wa fedha na upungufu wa waandishi wa miswada ya picha jongefu zinazotengenezwa, wakurugenzi, na wazalishaji wa vyombo vya habari waliobobea. Wataalamu hawa wanalazimika kutegemea teknolojia ya kizamani kutokana na gharama kubwa za vifaa vya kisasa.

Anaeleza kuwa ushindani kutoka kwa maudhui ya kigeni unadhoofisha simulizi za ndani. Pia anasema kuwa gharama za uzalishaji ni kubwa. [13]

**Rejea (vyanzo vyote mtandaoni vilipitiwa Machi 2025)**


1. https://www.osce.org/files/f/documents/0/f/91051.pdf.
2. https://documents.worldbank.org/pt/publication/documents-reports/documentdetail/129701468763468998/broadcasting-and-development-options-for-the-world-bank
3. Ibid. (kama ilivyotajwa juu).
4. TCRA. October-December 2024 Communications Statistics. https://www.tcra.go.tz/services/statistics
5. ttps://www.tcra.go.tz/documents/regulations
6. (Eltzroth, Carter & Kenny, Charles. (2003) in Broadcasting and development: Options for the World Bank.
7. [ Guidelines for Broadcasting Regulation. Second Edition. Eve Salomon. https://www.revistacomunicar.com/pdf/32/018-03-salomon.pdf
8. https://www.tcra.go.tz/documents/regulationTanzania.
9. https://www.tcra.go.tz/documents/rules
10. https://www.article19.org/data/files/pdfs/publications/africa-broadcasting-policy.pdf
11. Evaluation of Local Content Programming and Cultural Imperialism in Nigerian Broadcast Media. https://www.ajol.info/index.php/lwati/article/view/268238/2531196.
12. Imruh Bakari. Culture and Creative Industries in Tanzania. A Plan for Strategic Action. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000245149.locale=en
13. Wasilisho la Dr Elisha Magolanga kwenye mkutano wa mwaka 2025 wa utangazaji Tanzania ulioandaliwa na TCRA Dodoma Februari 2025. Lilihusu mikakati ya kuendeleza utengenezaji wa maudhui yenye ubora.




UTANGAZAJI

# Mikakati ya TCRA kuendeleza maudhui ya ndani

Na Mwandishi wetu

**Dondoo kutoka kwenye wasilisho la Mhandisi Andrew Kisaka, Meneja wa TCRA wa Huduma za Utangazaji kwenye Mkutano wa Mwaka wa Utangazaji uliofanyika Februari 2025 Dodoma.**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeandaa mkakati wa kukuza uzalishaji wa maudhui ya ndani yenye ubora wa juu katika utangazaji. Pia unahusu vipindi vinavyohusika na kukuza ubunifu na uvumbuzi.

TCRA inaamini kuwa ushirikiano wa wadau utasaidia kuunda mazingira yatakayoruhusu maudhui ya ndani kukuza utambulisho wa kitamaduni na uzalendo wa kitaifa.

Mkakati huu unalenga kuwawezesha waandishi wa simulizi za ndani, kuongeza ushirikishwaji wa watazamaji, na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Tanzania.

Dira ya TCRA kwenye mkakati huu ni kuwezesha televisheni na vyombo vya habari mtandaoni vya nchi kufikia viwango vya kimataifa.

Malengo makuu ni kuongeza wingi na ubora wa maudhui ya ndani, na pia kuunda, kuendeleza, na kukuza mazingira ambayo wazalishaji na waandishi wa maudhui wanaweza kustawi. Mfumo wa usimamizi, kupitia TCRA unahimiza uvumbuzi na kutumia teknolojia kwa ufanisi.

Mikakati mahsusi ya kukuza maudhui ya ndani inajumuisha uvishaji wa kifedha motisha za kikodi, ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi na ujenzi wa uwezo kupitia mafunzo na warsha.

Mafunzo hayo pia yatawawezesha watengenezaji wa maudhui kuwa na stadi za kushirikisha watazamaji.

Mikakati mingine ni pamoja na mpango wa uelekezaji, utaratibu wa kubadilishana uzoefu na matumizi ya majukwaa mbalimbali ya kusambaza na kutangaza maudhui.

Wadau ni pamoja na taasisi za Serikali yanayodhibiti na kusimamia maudhui na viwango, watangazaji, waandishi na wazalishaji wa maudhui na vikundi vya watumiaji.

Mashirika ya Serikali ni pamoja na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA), na Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TASUBA).




*Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa utangazaji, ulioandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania jijini Dodoma Februari mwaka huu.*

# Tanzania yajiandaa kuelekea utangazaji wa redio kidijitali

Na Mwandishi wetu

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imechapisha mpango wa matumizi ya masafa ya mawasiliano na mwongozo wa utangazaji wa redio kidijitali (DSB) ambao utaanza kwenye mikoa mitano.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri Bakari amesema wamealika maombi ya utoaji huduma za usambazaji wa maudhui chini ya mfumo huo wa utangazaji.

Dkt. Bakari amesema watoa huduma watakaoshinda zabuni watatumia teknolojia mbili za DSB zinazojulikana kitaalamu kama T-DAB+ na DRM30. Masafa yatakayotumika yako kwenye wigo wa megahezi (Mhz) 74-300 na kilohezi (Khz) 525-1605.

Mfumo wa kutoa huduma kwa utangazaji wa televisheni unatumika kwenye televisheni za kidijitali mfumo wa ardhini ambamo ving'amuzi vinatumika kupata huduma za maudhui.

TCRA imewapa hadi tarehe 9 Juni 2025 watoa huduma wanaokidhi masharti kuwasilisha maombi ya kutoa huduma hizo kwenye mojawapo ya mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza, au Mbeya. Mikoa hiyo inaongoza kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano Tanzania, hasa simu za mkononi.

Takwimu za TCRA wa hali ya mawasiliano kati ya Januari na Machi mwaka huu zinaonesha kuwa asilimia 42 ya laini zilizokuwa hewani nchini kote Machi 2025 zilisajiliwa mikoa hiyo mitano. Laini 90,298,941 zilikuwa hewani Tanzania Machi mwaka huu.




Dkt. Bakari ameeleza kuwa TCRA imeamua kuwa kila mkoa utakuwa na mtoa huduma mmoja kwa ajili ya ufanisi.

> "Ili kuongeza ufanisi katika matumizi ya masafa, TCRA kwa sasa imepanga kila eneo la huduma liwe na mtoa huduma binafsi mmoja atakayepewa leseni," amefafanua Dkt. Bakari.

Hii ni tofauti na kwenye mfumo wa utangazaji wa DTT ambako kuna watoa huduma watano kwa nchi nzima.

TCRA inasimamia utangazaji Tanzania Bara. Zanzibar inayo Tume ya Utangazaji. Taasisi hizi zinashirikiana kwenye maeneo mbalimbali.

Kwa kuanzisha utangazaji wa DSB Tanzania itakabili changamoto kuu mbili: masafa adimu ya utangazaji wa redio, hasa kwa huduma za maeneo ya mijini na umuhimu na haja ya kufikisha maudhui ya redio kwa hadhira pana zaidi. Redio 251 zilizokuwa na leseni za TCRA kufikia Machi 2025 zinatumia masafa ya FM, yanayoanzia wigo wa Megahezi 87.5 mpaka 108.

Kutokana na msongamano huo wa kidijitali, teknolojia za DSB zinakuja kwa wakati muafaka. Zinatumia masafa kwa ufanisi, zinahakikisha ubora wa sauti na zitawahakikishia wasikilizaji huduma bora popote watakapokuwa.

Vilevile DSB itafungua fursa za kusisimua kwa vituo vipya vya redio na huduma zitaenea zaidi na kufikia kila pembe ya Tanzania. Hadi Machi 2025, mawimbi ya redio ya FM yalifikia asilimia 81.5 ya Watanzania na yalienea kwenye asilimia 57 ya eneo la nchi.

## Rejea. Teknolojia ya DSB

DSB inawezesha kuenea mawimbi kuliko ilivyo kwa masafa ya AM na FM. Yanapanua uanuai wa maudhui na kufungua fursa za kuyatengeneza na kuyasambaza kwa hadhira pana zaidi.

Teknolojia ya T-DAB+ ilianza kama DAB kwa majaribio nchi za Ulaya miaka ya tisini. Ina ubora wa juu wa sauti na inatumia masafa kwa ufanisi zaidi kuliko mfumo wa awali wa DAB.

DRM ilianza China 1997 kudijiti masafa yaliyokuwa yanatumika. Mwaka 2005 iliboreshwa zaidi.

Nchi nyingi za Afrika zina mipango ya kuanzisha huduma za utangazaji wa redio kidijitali. Jumuiya za ushirikiano wa kiuchumi zimesawanisha mipango yao kuhusu DSB.

Hizi ni pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Ushirikiano Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Uchumi Afrika Magharibi (ECOWAS).

Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza Mashariki na Kusini mwa Afrika kuhamia mfumo wa utangazaji wa televisheni kidijitali mfumo wa ardhini (DTT) mwaka 2014.

Ilizima mitambo ya televisheni ya analojia Desemba 2014, miezi sita kabla ya tarehe ya mwisho ya Juni 2015 iliyokubaliwa kimataifa.

Hadi Machi 2025, DTT ilienea miongoni kwa watu Tanzania kwa asilimia **58** na kijiografia nchini kwa asilimia **33**.




*Wadau mbalimbali wakishiriki mkutano wa mwaka wa vyombo vya utangazaji nchini uliofanyika jijini Dodoma. Matumizi ya teknolojia ya utangazaji ya kidijitali yatasaidia kuongeza upatikanaji wa maudhui kwa ubora na kufikia hadhira pana.*

TEKNOLOJIA

# Wataalamu wataka akili-unde itumike kupambana na ulaghai mitandaoni

Na Mwandishi wetu

Timu ya wataalamu wa masuala ya fedha wamependekeza kutumika kwa akili-unde/akili mnemba na teknolojia wezeshi za kisasa kupambana na uhalifu mitandaoni, hasa kwenye mitandao ya simu za mkononi.


Mapendekezo hayo yametolewa hivi karibuni kwenye kikao-kazi cha wajumbe wa kamati ya wataalamu inayoshughulikia masuala yakuimarisha huduma za kifedha Tanzania. Kamati hiyo iko chini ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT).

Akili-unde au akili mnemba (AI) ni teknolojia ya kuanzisha mifumo ya kompyuta ambayo inaweza kufanya shughuli ambazo kwa kawaida zinafanywa na binadamu. Teknolojia wezeshi ni pamoja na ile inayofanikisha ufuatiliaji taarifa katika kanzidata zilizounganishwa.

Mapendekezo yao yanakuja sambamba na kutolewa kwa ripoti ya hali ya mawasiliano Tanzania kati ya Januari na Machi 2025 ambayo inaeleza kuwa akaunti za pesa kwa simu zimeongeka mara mbili ndani ya miaka minne.

Ripoti hiyo, iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Dkt. Jabiri Bakari inasema kiwango cha kukua akaunti za pesa kwa simu kilizidi cha usajili wa laini za simu kati ya Machi 2021 na Machi 2025.

**Akaunti za pesa kwa simu ziliongezeka kwa asilimia 103.4 kati ya Machi 2021 na Machi 2025)**




Laini za simu 90,298,941 zilikuwa zinatumika Machi 2025, kulinganisha na 52,813,930 Machi 2021, ongezeko la asilimia 71.

Ripoti hiyo pia inaonesha kuwa matukio ya ulaghai mitandaoni yaliyoripotiwa yaliongezeka kwa asilimia 33 kati ya Desemba 2024 na Machi mwaka huu. Kulikuwa na matukio 17,152 katika robo mwaka ya Januari-Machi 2025 ikilinganishwa na 12,896 Oktoba-Desemba mwaka jana.

Mikoa ya Morogoro na Rukwa bado inaongoza kwa kuvuma vibaya kwenye matukio ya ulaghai, ikiw na asilimia 74 ya matukio yote yaliyoripotiwa nchi nzima. Matukio 7,385 yaliripotiwa Rukwa na 5,227 Morogoro.

Wachambuzi wanasema kuongezeka kwa matukio yaliyoripotiwa kunaweza kuwa ni matokeo ya kampeni za kupanua uelewa wa watumiaji wa huduma za mawasiliano na wananchi kwa ujumla kwenye usalama mitandaoni.

TCRA inaendesha kampeni ya elimu kuhusu njia za kujilinda mitandaoni na umuhimu wa kuripoti ulaghai kwa kutuma ujumbe kwenye namba 15040 bure.

Kanzidata nyingi kwenye mfumo wa matumizi ya simu kwa njia mbalimbali zimeunganishwa. Huduma za pesa kwa simu zinasimamiwa na TCRA, ambayo inatoa leseni kwa watoa huduma za mitandao na kuwapa misimbo inayotumika kufanya miamala ya simu na benki. BOT inasimamia sekta ya fedha.

Aidha watumiaji wanasajiliwa kutumia alama za vidole na taarifa zilizoko Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Vifaa wanavyotumia vina namba tambulishi ya pekee ambayo inahifadhiwa kwenye rajisi kuu ya namba tambulishi (CEIR).

Huduma za pesa kwa simu za mkononi Tanzania zinatolewa na watoa huduma sita ambao wanatumia majina ya biashara ya Airtel Money, Azam Pesa, Halopesa, Mixx (zamani Tigopesa), M-pesa na T-Pesa.

MAPYA KWENYE SHERIA NA USIMAMIZI

# Kanuni zaboreshwa kuleta ufanisi utoaji huduma

Na Mwandishi wetu

Kanuni tano za mawasiliano ya kielektroniki na Posta zimeboreshwa ili kuimarisha ufanisi wa watoa huduma na kuinua ubora.  Maboresho hayo, yaliyochapishwa kwenye tovuti ya TCRA: www.tcra.go.tz, yanataka watoa huduma kuwa na mikataba na wateja wao wakubwa na watumiaji wa kawaida wa huduma zao.

Kanuni hizo pia zimetoa nafuu kwa wenye leseni ambao sasa wanatakiwa kuwasilisha taarifa zao za mahesabu wiki tatu baada ya kila robo mwaka badala ya wiki mbili za awali.

Mfumo wa utoaji leseni wa TCRA una leseni za ujenzi na uendeshaji wa miundombinu na mitandao ya mawasiliano, utoaji huduma kutumia mitandao, mifumo na programu tumizi na maudhui ya utangazaji. Mamlaka pia inatoa leseni za Posta na usafirishaji vifurushi.

Utangazaji unahusisha redio, televisheni na vyombo vya habari mtandaoni. Leseni za kielektroniki zinatolewa kwa huduma kitaifa, kiwilaya, na kwa jamii husika.

TCRA pia inasimamia huduma mbalimbali za mawasiliano na matumizi ya raslimali kama vile namba na masafa. Aidha inaidhinisha vifaa vya mawasiliano vinavyoingizwa na kutumika Tanzania.

Hivi karibuni, TCRA imeanzisha maabara maalumu jijini Dar es Salaam kuhakiki viwango vya ubora wa vifaa vya mawasiliano ili kuhakikisha ni salama na vinakidhi vigezo vya matumizi.

Mikataba ya wateja inatakiwa kuainisha kiwango cha chini cha utendaji kwa huduma zinazotolewa. Aidha iweke wazi njia za kufuatilia na kuthibitisha viwango vya utendaji husika kama vilivyoahidiwa kwenye mikataba.

Vilevile mikataba hiyo inatakiwa kuonesha bei na tozo kwa kila huduma na kutaja mifumo ya kutoa huduma nyingine wezeshi.

Aidha, mikataba itaje suluhisho au fidia kwa wateja kwa huduma ambazo hazitakidhi matarajio yao.

Kanuni za Posta zinataka watoa huduma kuwapatia wateja wao sera wanazowasilisha TCRA kuhusu fidia kwa upotevu au uharibifu wa vitu vinavyopostiwa.

Kanuni za Usalama Mitandaoni zinataja leseni mpya ya huduma za usalama mitandaoni. Leseni hiyo iko kwenye kundi linalokuwa na masharti mahsusi kwa mtoa huduma.

> "Kanuni za maudhui mtandaoni zinataka mwenye jukwaa la mtandao wa jamii kuhakikisha kwamba anakuwa na njia za kuchuja na kuzuia maudhui yaliyokatazwa mtandaoni na namna ya kuyaondoa.

Kanuni mpya za maudhui mtandaoni zimeongeza kwenye orodha ya maudhui yaliyokatazwa mtandaoni maudhui yasiyo na maadili, ya kutunga na yanayotengenezwa kwa kutumia akili-unde/akili mnemba. Haya ni pamoja na video, picha za kawaida na katuni.

Wakati huo huo TCRA imechapisha kanuni za kushughulikia vitu vya posta na vifurushi ambavyo kwa namna moja au nyingine havichukuliwi na waliotumiwa.

Kanuni zilizorekebishwa zimechapishwa kwenye tovuti ya TCRA kwenye kiungo:

1. https://www.tcra.go.tz/documents/regulations
2. https://www.tcra.go.tz/documents/rules.

# Mwelekeo ukuaji sekta kupita malengo ya Serikali

Na Mwandishi wetu

Ripoti ya hali ya mawasiliano Tanzania kati ya Januari na Machi 2025 inaonesha ukuaji maeneo mengi unakaribia kufikia na kupita malengo Serikali iliyojiwekea kwa kipindi cha miaka mitano kinachoisha Novemba mwaka huu.

Laini zinazotumika kwenye mitandao ya simu zimeongezeka kwa asilimia 35 kati ya Septemba 2023 na Machi 2025 nchi nzima na kwa asilimia 41 kwenye mikoa minne.

Kulikuwa na laini 90,298,941 nchini kote Machi 2025 ukilinganishana na 67,024,338 Septemba 2023. Huduma za intaneti zimeongezeka kwa asilimia 67 ndani ya miaka minne.

Uzao wa tano wa simu za mkononi 5G ulifikia asilimia 23 ya watu na kuenea kwa asilimia 3.6 kijiografia nchini Machi mwaka huu.

**5G**

Uzao wa tano wa simu za mkononi 5G ulifikia asilimia 23 ya watu na kuenea kwa asilimia 3.6 kijiografia nchini Machi mwaka huu.

5G ina ufanisi zaidi na inawezesha mifumo na programu tumizi zinazohitaji kasi kubwa ya data mitandaoni na ambayo inaunganisha na kuwezesha kutumika vifaa vingi kwa mara moja.

Gharama na tozo za maongezi ya simu za mkononi na matumizi ya data zimebakia zilivyokuwa Juni 2024.

Wachambuzi wanasema miundombinu mipya na iliyoboreshwa na ongezeko la leseni za huduma wezeshi vimechangia ukuaji huu.

Aidha ripoti inaonesha kuwa watoa huduma za utangazaji wanazidi kuzingatia matakwa ya kanuni kuhusiana na maudhui ya ndani. Vilevile wenye leseni za huduma za Posta na usafirishaji vifurushi wameongeza ubunifu ili kuongeza ufanisi, na wamechangamkia fursa zinazotokana na biashara mtandao.

Makala zifuatazo zinawasilisha yaliyojitokeza kwenye ripoti hiyo.

## Intaneti yaenea asilimia 72 miongoni kwa watu

Huduma za intaneti zimeenea asilimia 72 miongoni mwa watu Tanzania kufikia Machi 2025, mwelekeo unaoashiria kuwa lengo la Serikali la asilimia 80 ifikapo mwisho wa mwaka huu litafikiwa.

Laini zinazotumiwa kwa intaneti ziliongezeka kwa asilimia 70, kati ya Machi 2021 na Machi 2025, kutoka 29,071,817 hadi 49,333,839.

Serikali ilipanga kuongeza watumiaji wa intaneti kufikia asilimia 80 ya watu Tanzania kati ya Novemba 2020 na Novemba mwaka huu.

Idadi ya watumiaji wa intaneti inakokotolewa kutoka laini zilizotumika kupata huduma hiyo ndani ya miezi mitatu ya mwisho wakati wa kufanya tathmini, bila kujali aina na teknolojia iliyotumika.

Vifaa vya mkononi vinapendelewa zaidi kupata huduma za intaneti na asilimia 99.6 ya watumiaji wanapata huduma kupitia simu za mkononi, vishkwambi au modemu.




*Mwakilishi wa mtoa huduma za usafirishaji wa vifurushi akitumia kifaa cha mawasiliano ya mkononi kinachochakata data (PDA). Vifaa hivyo vimefanikisha shughuli za Posta na usafirishaji vifurushi nchini.*

Teknolojia nyingine kama zile zinazounganisha waya wa faiba hadi nyumbani (FTTH) au ofisini (FTTO) zina watumiaji wachache, ingawaje zina kasi karibu mara tatu.

Uchambuzi wa ripoti hiyo unaonesha kuwa huduma za waya za faiba zilikua kwa asilimia 5.32 kati ya Desemba 2024 na Machi 2025, kutoka 83,203 waliounganishwa kwenye FTTH n FTTO hadi 91,625 kwa kundi hilo.

Wastani wa kasi ya kupakua data kupitia vifaa vya mkononi vinavyotumika kwa intaneti ya kasi ni megabaiti-kwa-sekunde (Mbps) 12.5 ukilinganisha na Mbps 35 kwa waya za faiba. Aidha, kasi ya kupakia data ni Mbps 10.8 na 31.8 mtawalia.

Watumiaji wa Tanzania wanatumia asilimia 10.9 tu ya uwezo uliopo wa intaneti kimataifa kwa mawasiliano ya kutoka na kuingia nchini.

Wanatumia gigabaiti-kwa- sekunde Gbps) 1,968 kati ya 17,200 zilizopo. Gbps 15,232 za mawasiliano ya kutoka na kuingia hazitumiki.

Serikali inatekeleza mipango ya kuendeleza miundombinu ya mawasiliano ya mkononi na uwezo wake kutumia teknolojia zenye kasi zaidi. Hii ni pamoja na kujenga na kuboresha minara ya kurushia mawimbi ya mawasiliano ya simu za mkononi.

Uzao wa tano wa simu za mkononi (5G) unazidi kupanuka nchini. Watumiaji wake waliongezeka kwa asilimia 12 kati ya Januari na Machi 2025, kutoka 1,002,665 kufikia 1,123,900.

## Miundombinu mipya yafanikisha mawasiliano mikoani

Serikali inakamilisha ujenzi wa minara ya mawasiliano ya simu 758 na kuboresha mingine 300 nchini kote ili iwezesha utoaji huduma kwa teknolojia ya uzao wa tatu, wa nne na wa tano wa mawasiliano ya simu kwa vifaa vya mkononi (3G,4G na 5G).

Kuenea minara ya mawasiliano ya simu za mkononi na mitambo ya kurushia mawimbi vimewezesha laini zinazotumika nchini.

Usajili wa laini za simu uliongezeka kwa asilimia 41 mikoa ya Kagera, Kigoma, Tabora na Tanga kati ya Septemba 2023 na Machi mwaka huu.

Ongezeko la laini kati ya Septemba 2023 na Machi mwaka huu kwenye mikoa hiyo minne, na idadi kwenye mabano ni: Kagera (1,577,159 hadi 2,224,115), Kigoma (kutoka 1,279,021 mpaka 1,803,679), Tabora (kutoka 3,099,517 kufikia 4,371,032) na Tanga kutoka 2,365,189 hadi 3,335,396.

Mikoa hiyo pia ni miongoni mwa 12 yenye idadi kubwa ya mitambo inayowezesha mawasiliano ya 4G.


Teknolojia za juu zaidi za mawasiliano ya simu za mkononi yanaimarisha ubora wa maongezi na kuongeza kasi ya kutuma na kupokea data, hivyo kukidhi matarajio ya watumiaji.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) unasimamia mradi wa ujenzi na uboreshaji minara. Mradi huo ulizinduliwa 13 Mei 2023 na Rais, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia imejenga minara 42 Unguja na Pemba.

Kulikuwa na minara 9,278 Tanzania Machi 2025 kulinganisha na 8,551 in Juni 2024, ongezeko la asilimia 8.5.

Mikoa yote sasa ina angalau mnara mmoja wenye mitambo ya 5G. Mikoa iliyokuwa haina hadi Juni 2024 ni Mtwara, Lindi, Kaskazini Pemba na Katavi.



*Mojawapo ya minara ya mawasiliano ya simu za mkononi iliyojengwa maeneo ya vijijini Tanzania.*

Mikoa 10 inayoongoza kwa mitambo na idadi kwenye mabano ni: Dar es Salaam (633), Mjini Magharibi Zanzibar (60), Dodoma (46), Mwanza (41), Arusha (34), Mbeya (16), ) Songwe (13) Morogoro (9), Pwani (9) na Kilimanjaro (8).

Teknolojia ya 5G iliingia Tanzania Septemba 2022.

Hadi Machi 2025 teknolojia zilienea miongoni mwa watu kama ifuatavyo: uzao wa pili (2G) asilimia 98.4, 3G asilimia 92.2, 4G asilimia 90.7 na 5G asilimia 23. Kuenea kijiografia kulikuwa asilimia 76.2, 74.3, 73.3 na 3.6, mtawalia.

## Bei za huduma za mawasiliano zaendelea kuwa chini

Bei za huduma za mawasiliano Tanzania zimeendelea kuwa chini na kutokubadilika ndani ya miezi tisa huku mmoja wa watoa huduma akitoza asilimia 33 chini ya wengine. Vifurushi vya maongezi ya simu zimebakia shilingi 26 kwa dakika kwa mtandao wa mtumiaji na 28 kwa mtandao mwingine kuanzia Juni 2024 hadi sasa.

Tanzania ina watoa huduma za simu za mkononi watano – Airtel. Halotel, Yas (zamani TIGO), TTCL na Vodacom.

Bei za data pia zimebakia shilingi 9.35 kwa megabaiti (Mb) moja.

Gharama za kupiga simu nchi nyingine Afrika Mashariki zimeongezeka kwa asilimia tano (5), kutoka shilingi 597.40 kwa dakika Juni 2024 mpaka 627 Machi mwaka huu.


Halotel inatoza bei ya chini zaidi kwa simu nje ya vifurushi – shilingi 10 kwa dakika kwa mtandao wa mtumiaji na 20 kwenda mtandao mwingine.

Watoa huduma wengine wanatoza shilingi 30 kwa dakika ndani ya mitandao na kwenda mitandao mingine bila vifurushi na kati ya shilingi nane (8) na 10 kwa ujumbe mfupi, yaani meseji.

Ripoti inaonesha mwenendo wa kupanda na kushuka kwa baadhi ya huduma na matumizi yake. Kwa mfano dakika za maongezi ya simu za ndani zilipungua kwa wastani wa asilimia 4.5 kati ya Desemba 2024 na Machi mwaka huu, kutoka dakika bilioni 42.5 mpaka bilioni 40.6.

Dakika ndani ya mitandao zilipungua kwa asilimia 3.7, kutoka bilioni 21 Desemba 2024 mpaka bilioni 20.2. Kwenda mitandao mingine zilipungua kwa asilimia 5.3, kutoka bilioni 21.5 mpaka bilioni 20.4.

Watoa huduma za simu za mkononi na idadi ya laini walizosajili kwenye mabano ni: Airtel (23%), Halotel (14.7%), Yas (28.5%), TTCL (1.9%) and Vodacom (31.9%).




## Leseni za miundombinu zaongezeka asilimia 26 ndani ya mwaka

Leseni za miundombinu ziliongezeka kwa asilimia 26 kati ya Machi 2024 na Machi mwaka huu, kutoka 35 hadi 44.

Leseni nyingine, na ongezeko kwenye mabano ni: huduma za mtandao wa mawasiliano (kutoka 14 hadi 18), mifumo na programu tumizi (kutoka 135 mpaka 144), na Posta na usafirishaji wa vifurushi (kutoka 134 mpaka 151.

Vyeti vya idhini ya vifaa kutumika Tanzania viliongezeka kwa asilimia 124.5, kutoka 2,281 mpaka 5,120.

Vituo vya redio zimeongezeka kutoka 231 hadi 250, televisheni za mfumo wa ardhini zisizolipiwa sasa ziko 38 na televisheni za kulipiwa zimetoka 25 mpaka 31.

## Tanzania yajizatiti kupanua huduma za posta

Tanzania imeimarisha sera ya Posta, imeboresha kanuni na imeunganisha mfumo wa anwani za makazi na postikodi (NAPS) na mifumo mingine ya utoaji huduma kwenye taasisi 18.

Ripoti inasema NAPS imefungua fursa za biashara na utendaji kwa kuwezesha ufikishaji wa vitu majumbani, ofisini na sehemu za kazi.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilisema kwenye taarifa ya hivi karibuni kuwa anwani milioni 12.8 zilishasajiliwa kwenye mfumo wa NAPS hadi Machi 2025.

NAPS unafanikisha ufikishaji na uchukuaji wa vitu kutoka majumbani na maofisini na pia unawezesha Serikali na wakala wake kutekeleza mipango na kuwasiliana na wananchi kwa ufanisi.

Mfumo huu pia unaimarisha usalama, ustawi na mipango ya kueneza na kufikisha huduma muhimu. Inafanikisha huduma za dharura kama vile za magari ya wagonjwa, polisi na zimamoto na uokoaji.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt Jabiri Bakari amesema wataendelea kuhimiza matumizi na teknolojia za kisasa za ufuatiliaji ili kuwezesha watoa huduma za Posta na usafirishaji vifurushi kuboresha utendaji wao na kuhudumia wateja wao kwa ufanisi zaidi.

Ripoti ya Wizara imeeleza kuwa kuenea vifaa vya mawasiliano vya mkononi vinavyochakata data (PDA) kumefanikisha shughuli za Posta na usafirishaji vifurushi.

Vifaa hivyo vinawezesha taarifa kusafirisha kwa wakati mmoja taarifa kutoka sehemu za kuchukua au kufikisha vitu vya posta, vikiwemo mizigo, nyaraka na vipeto, kwenda kwenye mifumo mingine.

Ripoti inaonesha kuwa PDA 51,530 zilikuwa zimeunganishwa kwenye mitandao ya mawasiliano Tanzania Machi 2025.

Watoa huduma za Posta na usafirishaji vifurushi duniani kote wanapanua shughuli zao ili kuendana na mabadiliko ya kasi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Pamoja na huduma zilizokuwa zinatolewa na Posta kuchukuliwa na TEHAMA, watoa huduma wengi wamebuni mipango ya kutumia TEHAMA kufanikisha shguhuli zao.

Eneo linalojitokeza kwa kasi ni biashara mtandao, ambamo vitu vinavyoagizwa kielektroniki vinabidi kufikishwa au kuchukuliwa kwenye makazi, ofisini au sehemu za kazi za wateja.

Kanuni za Posta Tanzania zilirekebishwa 2024 na kuanzisha makundi matano ya postikodi. Kuna Postikodi za maeneo ya kiutawala, Posta, watumaji wakubwa wa barua, nyaraka na vipeto, maeneo makuu, na za muda kwa matukio au shughuli mbalimbali.




*Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan akikabidhiwa bango la anwani ya ofisi yake kwenye kikao kazi cha wakuu wa mikoa kuhusu mfumo wa anwani za makazi na postikodi.*

# Sekta ya Mawasiliano katika namba

## Miezi mitatu ya ukuaji wa kihistoria sekta ya mawasiliano Tanzania

### Watumiaji wa huduma wazidi kuongezeka


**86.8** Milioni — Desemba 2024

4.1% ▲


**90.4** Milioni — Machi 2025

Ongezeko hilo la watumiaji wa huduma za simu imefanya ueneaji wa huduma hizo kufikia **132.6%**

### Mgawanyo wa soko kwa watoa huduma hadi Machi 2025




### Laini za simu mpya takriban milioni 14 zasajiliwa ndani ya miezi 10






### Watu wengi zaidi wapata intaneti

Idadi ya watumiaji wa intaneti imeongezeka kwa **2.7%** ndani ya miezi mitatu

**48** Milioni — Desemba 2024

**49.3** Milioni — Machi 2025

### Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya mawasiliano

| | 2G | 3G | 4G | 5G |
|---|---|---|---|---|
| Desemba 2024 | 98.2% | 91.0% | 88.0% | 20.0% |
| Machi 2025 | 98.4% | 92.2% | 90.7% | 23.0% |

# Mamilioni waendelea kunufaika na huduma za pesa mtandao


## Akaunti za pesa mtandao zapaa

**Milioni 63.2** Desemba 2024

**4.1%** ▼

**Milioni 66.5** Machi 2025

## Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao




## Huduma za utangazaji kwa ufupi

Azam Media Limited ilikua na idadi kubwa ya visimbuzi vya DTT na DTH vilivyolipiwa vifurushi ikilinganishwa na watoa huduma wengine, ikifuatiwa na Star Media Limited.

Hadi **Machi 2025** kulikuwa na visimbuzi

**2,057,145**

vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha **miezi mitatu**

**26.2%** Huduma za televisheni kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT)

**73.8%** Huduma za televisheni kwa njia ya setelaiti (DTH)

### Ueneaji wa huduma za utangazaji kufikia Machi 2025

- **58%** ya watu waliofikiwa na mawimbi na DTT
- **100%** ya watu waliofikiwa na mawimbi na DTH
- **81.45%** ya watu waliofikiwa na mawimbi ya redio za FM
- **33%** ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTT
- **100%** ya eneo lililofikiwa mawimbi na DTH
- **56.95%** ya eneo lililofikiwa na mawimbi redio za FM


## Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa

**41,966 (62.3%)** Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kwa mtoa huduma TPC

**25,495 (37.7%)** Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto



### Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi/vipeto



Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
14414 Dar es Salaam, Tanzania.
Email: dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania